

Ujauzito na Mikanda ya Usalama ya Gari

- Mwanamke mjamzito anapaswa kuvaa mkanda wa mapajani chini ya tumbo, chini kwenye nyonga kadri iwezeka-navyo na kwenye sehemu ya juu ya mapaja.
- Mkanda wa mabegani unapaswa kukaa katikati ya matiti. Hakikisha mikanda inashika vizuri.

Makosa ya Kawaida ya Usalama wa Kiti cha Gari

- Kumgeuza mtoto kutoka kwenye kiti cha gari cha usalama kinachotazama nyuma kwenda kwenye kiti cha usalama kinachotazama mbele haraka sana.
- Kiti cha usalama hakijabanwa vya kutosha — hakifai kusonga zaidi ya inchi moja kutoka upande mmoja hadi mwingine au kutolewa kutoka kwenye kiti katika njia ya mkanda.
- Mkanda kwa mtoto haujakaza vya kutosha — iwapo unaweza kubana sana vifaa vya mkanda, umelegea sana.
- Kibanio cha kufunga kiko juu sana au chini sana — kinapaswa kuwa kwenye usawa wa kwapa la mtoto.
- Mtoto yuko kwenye kiti cha usalama kisicho sahihi — usimharakishe mtoto wako kwenye mkanda wa usalama
- Tumia KOMEO au mkanda wa usalama ili kumkinga mtoto mchanga, kiti kinachobadilishika au kinachotazama mbele, lakini sio vyote kwa pamoja.

Sheria ya Mkanda wa Usalama ya New York

- **Abiria wote** lazima wavae mkanda wa usalama kwenye gari bila kujali ukaaji na umri.

Usalama wa Abiria Watoto wa New York na Sheria ya Kiti cha Busta

- **Watoto chini ya umri wa miaka 2 lazima watumie kiti kinachotazama nyuma.**
- Watoto wote hadi umri wa miaka 8 lazima wazuiwe katika kiti cha mtoto cha usalama kilichothibitishwa.
- Inashauriwa kumweka mtoto kwenye kiti saidizi kulingana na urefu na uzito wake, badala ya umri wao.



Novemba 2020

Usalama wa Abiria Mtoto

- Viti vya gari lazima vikidhi viwango vya usalama wa magari vya serikali kuu na viwekwe vizuri ili kuzuia majeraha.
- Soma maelekezo ya mtengenezaji wa kiti cha gari na kijitabu cha mwongozo kwa mtumiaji wa gari ili kuhakikisha kiti cha usalama kinatumika na kimewekwa kwa usahihi.
- Fuata maelekezo kwa makini.
- Angalia kijitabu cha maelekezo ya kiti cha gari kwa ajili ya makatazo ya uzito na urefu kwa kila kiti cha gari.

NENDA POLEPOLE

WATOTO WENGI HUSONGEA KWENYE KITI KINACHOFUATA CHA GARI AU KWENYE KITI KISAIDIZI HARAKA SANA.

[NHTSA.gov/TheRightSeat](https://www.nhtsa.gov/TheRightSeat)

1 Kiti Kinachotazama Nyuma



- Kuna aina 3 za viti vya gari vina-
vyotazama nyuma; viti vya watoto wa-
changa, viti vinavyobadilishika na viti
vyenye mambo yote.
- Sheria ya NYS inataka watoto wote
wenye umri chini ya miaka 2 lazima
watumie kiti kinachotazama nyuma.
- Watoto wanaweza kukaa kwa muda
mrefu wakitazama nyuma kwenye viti
vya gari vinavyobadilishika kulingana
na ukomo wa urefu na uzito wa kiti.
- Kila mara weka viti vya usalama vina-
vyotazama nyuma katika mkao wa
kujinyoosha (pembe ya nyuzi 45) na
kwa mujibu wa maelekezo ya
mtengenezaji wa kiti cha gari.
- Hakikisha kishikizo cha mikanda ki-
meshika vizuri na kwenye au chini ya
mabega.
- Viti vinavyotazama nyuma vinapaswa
kuwekwa kwenye kiti cha nyuma cha
gari. Ikiwa kiti cha gari lazima kitumike
kwenye kiti cha mbele, mifuko ya hewa
lazima izimwe.
- Kamwe usiweke kiti cha gari kinacho-
tazama nyuma mbele ya mfuko wa he-
wa unaofanya kazi.

2 Kiti Kinachotazama Mbele



- Aina ya viti vinavyotazama mbele vyenye
lijamu ni viti vinavyobadilishika, vya
muunganiko na viti vyenye mambo yote.
- Angalia maelekezo ya mtengenezaji kwa
ajili ya uwekaji sahihi.
- Kwa watoto ambao wamepita kiti cha
kutazama nyuma: Watoto wanapaswa
kutumia viti vyenye lijamu
vinavyotazama mbele hadi wanapopita
ukomo wa uzito (mara nyingi pauni 40-
80).
- Weka kiti kinachotazama mbele kwa
wima na kwa mujibu wa maelekezo ya
mtengenezaji.
- Sogeza kishikizo cha mkanda kwenye
matundu sahihi katika au juu ya
mabega na hakikisha mikanda imeshika
vizuri.

3 Kiti cha Busta



- Watoto lazima watumie kiti kisaidizi
baada ya kupita matumizi ya kiti
kinachotazama mbele chenye lijamu na
wataendelea kutumia kiti kisaidizi hadi
watakapotoshea kwenye mkanda wa
usalama wa watu wazima.
- Viti vyote visaidizi vya chini na juu
lazima vitumike pamoja na mkanda na
mkanda wa begani.
- Viti visaidizi vinafanya mkanda ukae
vizuri kwenye nyonga ya mtoto na
mkanda wa begani kwenye sehemu
sahihi.
- Baadhi ya viti visaidizi vina egemeo
refu na vingine vinakuja bila egemeo.
- Viti visaidizi ambavyo havina egemeo
lazima vitumike kwenye magari yenye
sehemu ya kuegemeshea kichwa.

4 Mkanda wa Usalama wa Mtu Mzima



- Mtoto wako yuko tayari kutumia kiti cha mtu mzima pindi anapoweza
kukaa na kuegemea nyuma ya kiti cha gari, na magoti kujikunja kwenye
ukingo wa kiti cha gari bila kujikokota.
- Mkanda unapaswa kupita begani (sio shingoni), na mapajani (sio tumboni).
Hii kwa kawaida ni karibu 4'9".